

Jina \_\_\_\_\_ TAREHE: \_\_\_\_\_

Jinsia:

Mume

Mke

Jina la kaunti \_\_\_\_\_ kaunti ndogo \_\_\_\_\_

Jina la shule \_\_\_\_\_

VIWANGO VYA KUTATHMINI

	Kuzidisha matarajio	Kufika matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
SEHEMU (1) Kusikiliza na kuongea	Alama (4) 13 - 15	Alama (3) 10 - 12	Alama (2) 5 - 9	Alama (1) 0 - 4
SEHEMU (2) Kusoma	9 - 10	6 - 8	4 - 7	0 - 3
SEHEMU (3) Sarufi	13 - 15	10 - 12	5 - 9	0 - 4
SEHEMU (4) Jumla	35 - 40	26 - 32	14 - 25	0 - 11
Mwalimu				

### Maagizo

1. Tathmini hii ina sehemu tatu; kusikiliza na kuzungumza, kusoma na sarufi
2. Jibu maswali yote kulingana na maagizo.
3. Tumia lugha ya kiswahili kujibu maswali yote.

### SEHEMU YA KWANZA

#### KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(Alama 15)

1. (a) Toa majibu ya salamu hizi (alama 2)
  - (i) Alamsiki \_\_\_\_\_
  - (ii) Sabalkheri \_\_\_\_\_
- (b) Tamka maneno yafuatayo. Lipigie neno mstari ukisikia sauti /kw/ (alama 2)

kiwi      kwetu      karibu      kwingi
- (ii) Chagua maneno ambayo ni vitanza ndimi (Alama 3)
  - (a) dada na kaka
  - (b) mama na baba
  - (c) baba na papa
  - (d) kuku na gugu
  - (e) chai na mandazi
  - (f) pata na bata
  - (g) kiatu na soksi

#### Andika hivyo vitanzandimi hapa chini

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

#### (c) Tegua vitendawili (Alama 3)

- (i) Huku ng'o na kule ng'o \_\_\_\_\_
- (ii) Jicho la Mungu linachoma \_\_\_\_\_
- (iii) Sijui aendako wala atotako \_\_\_\_\_

#### II. Soma sentensi hizi. Tumia maneno ya heshima baadala ya yale yaliyopigiwa mstari.

(Alama 5)

- (i) Kukojoa kando ya barabara ni hatia.
- (ii) Nikifika nyumbani nitaenda kunya chooni.
- (iii) Mama mwenye mimba amezaa.
- (iv) Alipoketi kwenye vumbi alichafua matako.
- (v) Ndugu yake alikuwa anahara sana.

## SEHEMU YA PILI

### KUSOMA (Alama 10)

#### Soma habari hii kisha ujibu maswali yafuatayo.

Hapo zamani za kale wanyama wote ambao hula nyasi na majani waliishi pamoja. Waliishi katika msitu na walikuwa na afya njema.

Wanyama hawa walianza kuzaana na kuwa wengi. Miti nayo ikaanza kuwa michache na mvua kupungua. Wanyama walikosa chakula na hawakujua wafanye nini.

Ndovu alisema wapande miti kwa sababu miti italeti mvua, mvua nayo italeti majani mengi na nyasi. Wanyama walikubaliana kupanda miti kumi mwezi wa Januari. Walichota maji na kunyunyizia miti kwa sababu ya kiangazi. Walipanda miti mitano Februari.

Mvua ilinyesha Machi na wanyama wakapanda miti ishirini. Mwezi wa Aprili wakapanda miti ishirini na mmoja. Mei na Juni miti kumi na sita. Julai miti mitano Agosti na Septemba hawakupanda miti yoyote. Oktoba na Novemba wakapanda ishirini na Desemba miti miwili. Mwaka huo wakapanda miti tisini na tisa. Waliendelea hivyo kila mwaka miti ikaongezeka, nyasi na majani vivyo hivyo. Mvua pia ikaendelea kunyesha.

#### Maswali

- a. Wanyama walikuwa wanakula \_\_\_\_\_ na \_\_\_\_\_
- b. Je, wanyama waliishi wapi? \_\_\_\_\_
- c. Ndovu pai huitwa \_\_\_\_\_
- d. Taja idadi ya miti iliyopandwa mwezi wa nne wa mwaka  
\_\_\_\_\_
- e. Mwaka huo walipanda miti tisini na tisa. Andika kwa idadi \_\_\_\_\_
- f. Taja faida moja ya kupanda miti kulingana na kifungu ulichosoma  
\_\_\_\_\_
- g. Ni miezi gani ambayo wanyama hawakupanda miti?  
(i) \_\_\_\_\_  
(ii) \_\_\_\_\_
- h. Ukosefu wa mvua huleta \_\_\_\_\_  
(masika, kipupwe, ukame, miti)

## SEHEMU YA TATU

### SARUFI

3. (a) Pigia mstari **nomino** katika sentensi. **(Alama 5)**
- (i) Wanafunzi wanapanda miti.
  - (ii) Daktari alimtibu mgonjwa.
  - (iii) Rais alihimiza tuwe na upendo.
  - (iv) James ni mwalimu bora wa Kiswahili.
  - (v) Kiatu changu ni kizuri.
- (b) Pigia mstari vivumishi katika sentensi **(Alama 3)**
- (i) Halima amevaa nguo nyeupe
  - (ii) Chumba cha mama ni safi.
  - (iii) Vipepeo wale ni maridadi.
- (c) Jaza nafasi kwa kutumia wingi wa nomino kwenye mabano **(Alama 3)**
- (i) Wanafunzi wameokota \_\_\_\_\_ (jiwe) uwanjani.
  - (ii) Hadithi za \_\_\_\_\_ (jitu) zinatisha.
  - (iii) Sebule imepambwa kwa \_\_\_\_\_ (ua) ya kupendeza.
- (d) Geuza sentensi hizi ziwe katika umoja **(Alama 2)**
- (i) Walimu walifundisha vizuri  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
  - (ii) Vipepeo wameruka kuelekea mashariki  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (e) Jaza nafasi kwa kutumia “u’ au “i” **(Alama 2)**
- (i) Mkeba \_\_\_\_\_ tachomwa.
  - (ii) Mipera \_\_\_\_\_ napaliliwa.